JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA KAHAWA TANZANIA

(Imeanzishwa kwa Sheria ya Kahawa Namba 23 ya Mwaka 2001 na Marekebisho ya Sheria za Mazao Na. 20 ya mwaka 2009)

TAARIFA KWA UMMA

MWONGOZO WA MASOKO YA KAHAWA KWA MSIMU WA KAHAWA 2021/2022

UTANGULIZI

Bodi ya Kahawa kwa mujibu wa Kanuni ya 63 ya Kanuni za Kahawa 2013 inatoa mwongozo mahsusi kuhusu utaratibu wa masoko ya kahawa kwa msimu wa kahawa 2021/2022 unaotarajiwa kuanza mwezi Mei 2021. Mwongozo huu unasomwa pamoja na mwongozo wa masoko ya kahawa uliotolewa na Bodi ya Kahawa Machi 2018 pamoja na mwongozo wa maboresho ya masoko ya kahawa uliotolewa Aprili 2019. Ifahamike kwamba, masuala yote ambayo hayakuelezwa katika mwongozo huu yataendelea kutekelezwa kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa awali.

1.1. MADHUMUNI YA MWONGOZO

Kuweka mazingira wezeshi katika mfumo wa masoko ya kahawa kwa wakulima, wafanyabiashara, na wadau wote kwa lengo la kuongeza ushindani, kuwezesha viwanda kupata malighafi, kupunguza malalamiko na ukiritimba usio wa lazima, kuimarisha bei ya mkulima, kuimarisha ushirika pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa ushuru kwa Halmashauri. Kwa kufanya hivi kutaongeza ustawi na tija ya sekta ya kahawa.

2.0. UTARATIBU WA MASOKO

Kutakuwepo na aina tatu za masoko ya kahawa, ambayo ni Soko la awali (Farm gate market), Soko la mnada wa kahawa na Soko la Moja kwa moja (Direct Export). Aina hizi za masoko zimetolewa ili kumpa mkulima wigo mpana wa kuchagua soko lenye manufaa zaidi kwake kwa kuzingatia bei, uharaka wa malipo na mabadiliko ya bei kwenye masoko ya kahawa na upatikanaji wa malighafi kwa wenye viwanda vya kuongeza thamani.

2.1. Soko la awali (Farm gate Market)

2.1.1. Ununuzi wa kahawa ghafi

Wanunuzi binafsi na wenye viwanda wanaruhusiwa kununua kahawa kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi au Vyama Vikuu (Union). Kahawa itakayonunuliwa katika soko hili ni ile ambayo imepitia utayarishaji ngazi ya awali (Dry Cherry na Parchment). Wanunuzi wa kahawa watakaotaka kununua kahawa katika soko hili watatakiwa kuwa na leseni za kununua kahawa zinazotolewa na Bodi ya Kahawa kwa mujibu wa Sheria ya Kahawa na Kanuni zake (Parchment Buyers Licence & Dry Cherry Buying Licence). Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kwa kuzingatia Kanuni Na. 26 (2) na Na. 38 (5) za Kanuni ya Kahawa ya mwaka 2013 watatoa vibali kwa wanunuzi wa kahawa kwenye Halmashauri zao ikiwa ni moja ya masharti ya kupata leseni ya ununuzi kutoka Bodi ya Kahawa.

2.1.2 Utaratibu wa kununua kahawa

i. Wanunuzi wa kahawa wanaotaka kununua kahawa watapaswa kwenda kwenye chama husika cha ushirika na kufanya makubaliano kwa kuingia mikataba ya uwazi juu ya kununua kiwango cha kahawa walichokubaliana.

ii. Bei itakayokubaliwa katika makubaliano ya manunuzi hayo ni lazima iwe bei shindani.

iii. Mnunuzi huyo atapaswa kulipa kwenye akaunti ya chama cha ushirika fedha za mauzo ya kahawa ndani ya siku tano za kazi baada ya makubaliano kukamilika na ni lazima chama kitoe risiti inayoonyesha mauziano hayo ya kahawa, Chama cha ushirika kitakuwa huru kumuuzia mnunuzi mwingine iwapo mnunuzi wa awali hajalipia. Mnunuzi atatakayechelewa kufanya malipo na kuvunja makubaliano atachukuliwa hatua.

iv. Mara baada ya kukamilisha malipo mnunuzi wa kahawa husika atakuwa huru kuipeleka kahawa kwenye kiwanda cha ukoboaji ngazi ya pili (*Secondary Processing)* alichokiainisha kwenye maombi ya Leseni ya Ununuzi wa Kahawa na kuiuza katika soko la mnada au kwa utaratibu wa soko la moja kwa moja.

ANGALIZO: Kahawa ambazo tayari zipo kwenye utaratibu wa watoa huduma hazitahusika katika utaratibu huu na endapo mnunuzi yeyote atapenda kununua atalazimika kurejesha kwanza fedha za mtoa huduma ili aweze kununua kahawa hiyo. Makubaliano ya kilimo cha mkataba ni lazima kusajiliwa na Bodi ya Kahawa kwa mujibu wa kanuni ya 59 (3) ya Kanuni za Kahawa, 2013. Chama cha ushirika chenye makubaliano na watoa huduma wengine kinapaswa kuweka wazi makubaliano hayo kabla ya kuingia makubaliano mapya na mnunuzi wa kahawa.

2.1.3 Malipo kwa wakulima

Ili kuondoa malalamiko ya wakulima kuchelewa kulipwa mazao yao, Vyama vikuu vya ushirika vinatakiwa kuvilipa vyama vya msingi/AMCOS malipo ya awali kwa kahawa waliokusanya ndani ya siku saba baada ya kahawa hiyo kuwasilishwa kwenye maghala ya chama kikuu. Iwapo kuna makubaliano mengine mf. Malipo ya kahawa yafanyike baada ya mauzo kukamilika ni lazima vyama vya ushirika kuweka makubaliano hayo wazi kwa wanachama wao.

2.1.4 Utoaji wa taarifa

Bodi ya Kahawa imepewa jukumu la kukusanya, kusafisha, kuhifadhi, kutumia au kusambaza taarifa na takwimu zinazohusiana na tasnia ya kahawa katika kifungu 5 (1) na (2) (c) cha Sheria ya Tasnia ya Kahawa ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2009. Hivyo basi, katika utekelezaji wa jukumu hili la kisheria, Bodi inavitaka vyama vyote vya ushirika vinavyojitegemea na vyama vikuu kuwasilisha taarifa za makusanyo, mauzo ya kahawa na malipo kwa wakulima wa kahawa kila mwezi. Vyama vyote vya ushirika vitawajibika kutoa taarifa hizi kwa Bodi bila shuruti. Pia wazalishaji binafsi wa kahawa (Coffee estates) wanapaswa kuwasilisha taarifa zao za uzalishaji wa kahawa kwenye ofizi za bodi zilizopo kwenye maeneo walipo.

3.0. SOKO LA MINADA YA KAHAWA

3.1. Minada ya Kanda

Kama ilivyokuwa katika misimu miwili iliyopita Bodi ya Kahawa itaendesha minada ya kahawa katika kanda za uzalishaji kama ifuatavyo:

i. Kanda za Mbeya/Songwe – Minada ya kahawa itafanyika Wilaya ya Mbozi katika ukumbi wa kiwanda cha kukobolea kahawa Mbozi (MCCCo).
ii. Kanda ya Ruvuma - Minada ya kahawa itafanyika katika Wilaya ya Mbinga katika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga.
iii. Kanda ya Kagera minada ya kahawa itafanyika pale Bodi itakapopokea kiasi cha kutosha kuendeshea minada na taarifa za sehemu ambayo minada ya kahawa itafanyika mtajulishwa.
iv. Kanda ya Kaskazini utaendelea kwa kuuza kahawa ya mikoa ya kanda ya Kaskazini na kahawa kutoka kwa wauzaji wengine watakaopenda kuendelea kutumia mnada huu.

Katika kipindi chote cha msimu minada itafanyika kila wiki siku ya Alhamisi na wauzaji katika kanda zote wataruhusiwa kuuza kahawa yao kwenye mnada wowote watakaopenda ili kuwahi mzunguko wa mnada. Viwanda vya kukoboa kahawa vitatakiwa kuwasilisha kwenye ofisi za kanda za Bodi ya Kahawa sampuli za kahawa pamoja na *warranti* angalau siku kumi kabla ya siku ya mnada ili kuiwezesha Bodi kufanya maandalizi ya minada.

3.1.1. Uwekaji wa bei ya akiba (Reserve price)

Kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji wa minada ya kahawa wauzaji wa kahawa wanaruhusiwa kuweka bei ya akiba (Reserve price) ya kuuzia kahawa yao kwenye mnada. Bei hii iwasilishwe Bodi ya Kahawa kabla ya mnada husika wa kahawa kufanyika. Wauzaji wa kahawa kwenye minada ya kahawa hawaruhusiwi kubadilisha bei ya akiba mara baada ya mnada husika kuanza na endapo bei ya akiba iliyowekwa haikufikiwa kwenye mnada huo kahawa hiyo itarudishwa na kuuzwa kwenye mnada unaofuata. Endapo muuzaji akiafiki bei ya juu iliyopatikana kwenye mnada, kahawa hiyo itauzwa kwa muuzaji aliyetoa bei hiyo.

Kama muuzaji hakuwasilisha bei ya akiba kwa ajili ya kuuzia kahawa yake, bei ya akiba iliyowekwa Bodi ndio itatumika kama bei ya akiba ya kuuzia kahawa hiyo. Aidha ili kuhakikisha kunakuwepo na ushindani wa kweli kwenye minada ya kahawa, wauzaji hawaruhusiwi kuwasiliana na wanunuzi na kukubaliana kuhusu bei nje ya mnada.

3.1.2. Uondoaji wa kahawa kwenye mnada

Wauzaji wa kahawa kwenye mnada wanaruhusiwa kuondoa kahawa (coffee withdrawal) kwenye mnada husika kwa kutoa taarifa ya maandishi Bodi ya Kahawa. Taarifa ya kuondoa kahawa husika kwenye mnada zinatakiwa kutolewa kabla ya kabrasha la mnada (Auction catalogue) kutolewa kwa wanunuzi na kwa mujibu wa taratibu za mnada hutolewa siku 7 kabla ya siku ya mnada. Haitaruhusiwa kuondoa kahawa kwenye mnada mara baada ya kabrasha la mnada na sampuli kusambazwa kwa wanunuzi kwa kuwa wanunuzi hufanya maamuzi ya kushiriki kwenye mnada husika baada ya kupata kabrasha la mnada.

3.1.3. Hitimisho la manunuzi kwenye mnada (Bid Confirmation)

Katika kuhakikisha kunakuwa na uwazi kwenye minada ya kahawa, wanunuzi wa kahawa kwenye mnada wataruhusiwa kufanya hitimisho la manunuzi (Confirmation of Bid) masaa mawili baada ya mnada kukamilika. Kahawa ambayo bei kinga iliyowekwa haikuweza kufikiwa itaondolewa na kuuzwa tena kwenye mnada unaofuata. Kwa namna yeyote haitaruhusiwa kufanya makubaliano ya bei kati ya mwenye kahawa na mnunuzi nje ya mnada.

4.0. SOKO LA MOJA KWA MOJA (DIRECT EXPORT)

Wauzaji wa kahawa wenye nia ya kuuza kahawa kupitia soko la moja kwa moja watalazimika kufanya tathmini ya bei, kati ya bei ya kahawa ya daraja hilo kwenye minada na bei waliyoahidiwa na mnunuzi (Offered price) kabla ya kuingia makubaliano ya ununuzi wa kahawa. Makubaliano ya kuuza kahawa kwenye soko la moja kwa moja yakishafikiwa na kusajiliwa na Bodi ya Kahawa yanatakiwa kuheshimiwa kwa mujibu wa sheria ya mikataba ili kulinda taswira ya sekta ya kahawa.

Aidha wanunuzi wa kahawa kwenye soko la moja kwa moja wao wenyewe au kupitia mawakala wao watalazimika kuwa wamewasilisha makubaliano ya ununuzi wa kahawa Bodi ya Kahawa kwa ajili ya usajili ndani ya siku 3 tangu tangu kusainiwa kwa makubaliano hayo. Aidha, wanunuzi hao watalazimika kulipa malipo ya mauzo ya kahawa ndani ya muda uliokubaliwa kwenye mikataba yao. Muuzaji anatakiwa kulipa ankara yake ya kibali cha kuuza kahawa nje ya nchi ndani ya siku saba.

Tafsiri ya kisheria ya soko la moja kwa moja (Direct Export) kwa mujibu wa kanuni na. 42 (5) na kipengele na. 2 cha Jedwali la Tano katika Kanuni za Kahawa, 2013, ni mauzo na usafirishaji wa kahawa (premium coffee) baina ya muuzaji aliyepo ndani ya nchi na mnunuzi aliyeko nje ya nchi na siyo vinginevyo. Mmiliki mwenye leseni ya kuuza kahawa katika soko la moja kwa moja (Direct Export Licence holder (D.E.) haruhusiwi kuuza kahawa kwa mnunuzi yeyote mwenye leseni ya D.E. aliyepo ndani ya nchi. Wauzaji wa kahawa kupitia soko la moja kwa moja wataruhusiwa tu kuuza kahawa kwa wanunuzi wa kahawa walio nje ya nchi kwa mujibu wa masharti ya leseni zao na/au kuuza kahawa yao kupitia soko la mnada kwa mujibu wa kipengele na. 8 cha Jedwali la Tano katika Kanuni za Kahawa, 2013.

5.0. MAHUSIANO KATI YA VYAMA VYA USHIRIKA NA WATOA HUDUMA KATIKA SEKTA YA KAHAWA (SERVICE PROVIDERS)

Kanuni ya 59 ya kanuni za kahawa 2013 inaruhusu wazalishaji kahawa (Vyama vya Ushirika) kuingia makubaliano na wawezeshaji (Financiers) kwa ajili ya kufanikisha shughuli za uzalishaji wa kahawa. Hivyo kwa mujibu wa kanuni hii pamoja na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, Vyama vya Ushirika vinaweza kuingia makubaliano ya kushirikiana na kampuni binafsi katika maeneo yafuatayo;

5.1. Shughuli za uzalishaji wa kahawa

Vyama vya Ushirika vinaweza kuingia makubaliano na kampuni binafsi kuwezeshwa kupatikana kwa huduma zifuatazo kwa wazalishaji;

i. Upatikanaji wa pembejeo hususani zinazowawezesha wakulima kuongeza tija na ubora wa kahawa.
ii. Upatikanaji wa mitaji (Prefinancing).
iii. Huduma za ugani hususani katika usimamizi wa ubora wa kahawa.

Makubaliano kati ya Vyama vya Ushirika na watoa huduma yataridhiwa na Ofisi ya Mrajisi kabla ya kuwasilishwa Bodi ya Kahawa kwa ajili ya kupitiwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria.

5.2. Huduma za gharama za masoko (Logistical support)

Viwanda vya kukoboa kahawa vinaruhusiwa kuingia makubaliano na kutoa huduma zitakazowezesha Vyama vya Ushirika kukusanya kahawa, kuitayarisha na kuipeleka sokoni. Huduma hizo ni pamoja na magunia, usafiri, utayarishaji, utunzaji na uhifadhi wa kahawa ghalani, utoaji wa mitaji n.k. Urejeshwaji wa gharama za huduma hizi utafanywa baada ya kahawa kuuzwa.

6.0. USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA VIWANDA VYA AWALI VYA KUCHAKATA KAHAWA (CPU)

6.1. Usimamizi wa CPU

Vyama vya Ushirika vinaweza kuingia makubaliano na mwezeshaji katika shughuli za usimamizi na uendeshaji wa CPU ambapo kahawa ya wakulima itakusanywa na chama husika na kuchakatwa katika CPU kwa usimamizi wa chama chenyewe na mwezeshaji walioingia makubaliano. Wakati wa utekelezaji wa makubaliano hayo mwezeshaji anaweza kutoa malipo ya awali kwa kahawa mbivu (Cherry) inayopelekwa kwenye kiwanda husika. Kahawa hiyo inaweza kuuzwa kwenye soko la mnada au katika soko la moja kwa moja (Direct export) kwa mujibu wa taratibu zilizopo kisheria na baada ya mauzo kukamilika wakulima watalipwa bei ya nyongeza inayotokana na ubora ulioongezeka (Premium).

6.2. Matumizi ya CPU zinazomilikiwa na makampuni binafsi

Vyama vya ushirika vilivyopo kwenye maeneo ambako kuna miundombinu na mitambo ya CPU inayomilikiwa na makampuni binafsi, vinaweza kuingia makubaliano ya kukodisha mitambo hiyo kwa ajili ya kuchakata kahawa za wakulima wao kwa nia ya kuongeza ubora wa kahawa yao. Makubaliano hayo yanaweza kuwa ya chama cha ushirika kukodisha miundombinu hiyo na kuiendesha yenyewe au kuendesha kwa ushirikiano kama ilivyoelezwa katika kipengele 6.1. ya mwongozo huu. Makubaliano ya kukodisha miundombinu hiyo ionyeshe gharama za ukodishaji kwa msimu, gharama za matengenezo ya miundombinu hiyo na utaratibu wa malipo ya ukodishaji. Aidha makubaliano hayo yanatakiwa kufanyika mapema ili kuwa na muda wa kutosha wa kufanya maandalizi ya uendeshaji wa miundombinu hii mara kahawa zinapokuwa tayari zimeiva.

7.0. UPATIKANAJI WA VYETI VYA KAHAWA ENDELEVU NA UTHIBITI (CERTIFICATION/VERIFICATION).

Vyama vya Ushirika vinaweza kuingia makubaliano ya kuwezeshwa katika usajili kwenye mifumo mbalimbali ya kahawa endelevu na uthibiti (certifications and verification) iliyopo nchini. Makubaliano hayo yaeleze gharama za uwezeshaji na utaratibu wa malipo ya bei ya nyogeza (Premium) utakuwa. Katika makubaliano hayo, cheti cha usajili katika mifumo hiyo kitabeba majina ya chama cha ushirika na kampuni husika (Joint Ownership). Kahawa husika itauzwa katika soko la mnada au kwa utaratibu wa soko la moja kwa moja (DE) kwa mujibu wa taratibu zilizopo kisheria.

8.0. UPATIKANAJI WA MALIGHAFI KWA WASINDIKAJI WA KAHAWA (WAKAANGAJI) WA NDANI.

Ili kuongeza kiwango cha kahawa kinachoongezwa thamani kwa ajili ya soko la ndani na kuuzwa kwenye soko la nje, wasindikaji wa kahawa watapata malighafi kwa ajili ya usindikaji kwa kupitia njia zifuatazo;

i. Kununua kahawa kwenye minada.
ii. Wazalishaji kahawa wenye mashamba ya kahawa wanaruhusiwa kusindika kahawa yao waliyoizalisha na kutoa taarifa kwenye Halmashauri husika na Bodi ya Kahawa.

Imetolewa na,

KAIMU MKURUGENZI MKUU,
BODI YA KAHAWA TANZANIA,
S. L. P 732, MOSHI.